


TEMBO-FARU wana haki ya kuishi Tanzania

Ulinzi wa wanyama kwa mtazamo wa Kikristo na Kiislamu

Ulinzi wa wanyama kwa mtazamo wa Kikristo na Kiislamu



REV. CHRISTOSILER P. KALATA
MWANDISHI WA KAMATI

TEMBO NA FARU WANA HAKI YA KUISHI TANZANIA

Ulinzi wa wanyama kwa mtazamo wa Kikristo na Kiislamu

Rev. Christosiler P. Kalata
Mobile: +255 713 298 686
E-mail: christosiler@yahoo.com
christosilerkalata@gmail.com

**KAMATI YA AMANI YA VIONGOZI
WA DINI MKOA WA DAR ES SALAAM**

Kimetolewa na:
Kamati ya Viongozi wa Dini
Mkoa wa Dar es Salaam (KVDMD)
S.L.P. 46121, Dar es Salaam

Kimepitiwa na:
GPL Books Publishers
S.L.P. 6804, Dar es Salaam - Tanzania
Mobile: +255 715 059 171 / +255 767 059 171

Hakimiliki

©Kamati ya Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Dar-es-Salaam (KVDMD)

Mwandishi:

©Rev. Christosiler P. Kalata
Mobile: +255 713 298 686
E-mail: christosiler@yahoo.com / christosilerkalata@gmail.com

Toleo la Kwanza 2016

ISBN: 978-9976-925-50-0

Hakuna sehemu yoyote ya kitabu hiki ambayo inapaswa kutolewa upya au kuhamishwa kwa namna au njia yoyote ile, yaani, kwa elektroniki, kiufundi, kwa kutoa nakala (photocopy), kwa kurekodi kwa namna yoyote ya kuhifadhi maandishi au habari au kurudisha tena, bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa Mwandishi wa kitabu hiki.

Kimechapishwa na:

Jamana Printers Ltd
S.L.P. 5584, Dar es Salaam, Tanzania

TEMBO NA FARU WANA HAKI YA KUISHI TANZANIA

Ujangili wa Tembo na Faru Tanzania lazima ukomeshwe



*Mchungaji Christosiler P.E. Kalata
Mwandishi wa Kamati-KAVDMD*

“The conservation of wildlife and wild places calls for specialists knowledge, trained manpower and money, and we look to other Nations to co-operate with us in this important task, the success or failure of which not only affects the continent of Africa but the rest of the world as well”

KAMATI YA AMANI YA VIONGOZI WA DINI MKOA WA DAR-ES-SALAAM



YALIYOMO

TABARUKI.....	VI-VII
DIBAJI	VII-XI
QUOTABLE QUOTES.....	XII
UTANGULIZI	XIII-XV
SHUKRANI.....	XVI
SURA YA 1: SIKU YA SITA YA UUMBAJI.....	1
SURA YA 2: KUUMBWA KWA MWANADAMU	15
SURA YA 3: VITA VYA KUPAMBANA NA UJANGILI... ..	27
SURA YA 4: WANYAMA WANA HAKI YA KUISHI	44
SURA YA 5: TANZANIA NA HAKATI ZA KUPAMBANA NA UJANGILI	57
SURA YA 6: MUNGU ANASIKITIKA	58
SURA YA 7: MIMEA	82
SURA YA 8: FEDHA: MTEGO WA SHETANI.....	103
SURA YA 9: HITIMISHO.....	105

TUPAMBANE NA UJANGILI



KINDNESS TO ANIMALS

“Mwenye baki huufikiri uhai wa mnyama wake; Bali huruma za mtu mwovu ni ukatili” Mithali 12:10

As we have seen, all animals are to be treated with respect and kindness. Unfortunately, in some Muslim communities these guidelines are not followed. Some people mistakenly believe that since humans needs take priority, animal rights are not an urgent issue. Others find excuses to mistreat certain animals, such as dogs. These actions fly in the face of Islamic teachings, and the best way to combat such ignorance is through education and good example. Individuals and governments have an important role to play in educating the public about the care of animals, and establishing institutions to support animal welfare.

“It is forbidden in Islam to treat an animal cruelly, or to kill it except as needed for food. The Prophet Muhammad often chastised his Companions who mistreated animals, and spoke to them about the need for mercy and kindness. Here are several examples of hadith which instruct Muslims about how to treat animals”

“Whoever is kind to the creatures of God, is kind to himself.” -The Prophet Muhammad

“And I will punish the world for their evil, and the wicked for their iniquity; and I will cause the arrogance of the proud to cease, and will lay low the haughtiness of the terrible” Isaih 13:11

“Mwenye haki huufikiri ubai wa mnyama wake; Bali huruma za mtu mwovu ni ukatili” Mithali 12:10

“Verily We created man from a product of wet earth; then placed him as a drop (of seed) in a safe lodging; then We fashioned the drop into a clot, then We fashioned the clot into a little lump, then We fashioned the little lump into bones, then clothed the bones with flesh, and then produced it another creation. So blessed be Allah, the Best of Creators!” [23:12-14]

“God said, See, I have given you every plant yielding seed that is upon the face of all the earth, and every tree with seed in its fruit; you shall have them for food.

And to every beast of the earth, and to every bird of the air, and to everything that creeps on the earth, everything that has the breath of life, I have given every green plant for food.

And it was so. God saw everything that he had made, and indeed, it was very good.” Genesis 1:29-31

DIBAJI



Ujangili wa Tembo na Faru Tanzania lazima ukomeshwe

“Nimekuwa nikijiuliza maswali mengi katika maisha yangu, I never thought to ask myself why God created the world. I had asked myself the question, “why did God create me specifically “ which seemed like a more practical thing to wonder. But the answers I found to that question always struck me as shallow. I think that’s because it’s impossible to understand what part we play in a story if we have never grasped what the story is about in the first place.”

Ninachokifahamu hadi sasa pengine kitabu hiki kinaweza kuwa kimoja cha vitabu vichache sana vilivyowahi kuandikwa na viongozi wa dini, wakiunganisha maandiko Matakatifu kutoka Biblia na Quran! Uumbaji una siri za Kimungu, ni pale mwanadamu anapokumbushwa na Mungu mwenyewe ndipo anapojitambua:

“Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe, Wala sitazikum buka dhambi zako. Unikumbushe, na tuhojiane Eleza mambo yako upate kupewa haki yako” Isaya 43:25-26

Kitabu hiki kitawafikia wengi, na kitatoa majibu yanayogusa maisha yetu, kimwili, kiakili, na kiroho. “ Tanzania imetajwa kwenye taarifa ya utafiti duniani iliyorushwa na kituo cha runinga cha CNN hivi karibuni kuwa nchi ya kwanza kwa kuvutia watalii wanaokuja kuangalia Wanyamapori Barani Afrika, ikifuatiwa na Botswana, Kenya, Zambia, Afrika Kusini, Namibia, Uganda, na Zimbabwe.

Idadi ya watalii kutoka nje wanaotembelea nchi yetu imeongezeka kwa asilimia 4 kutoka watalii 1,095,884 Mwaka 2013 hadi watalii 1,140,156 mwaka 2014, pamoja na kumekuwepo na changamoto za athari za gonjwa la Ebola Magharibi mwa Afrika, tishio la Ugaidi Ukanda wa Afrika Mashariki na kuporomoka kwa sarafu ya Euro Barani Ulaya.

Kwa mujibu wa taarifa rasmi ya Benki Kuu ya Tanzania, Utalii sasa unaongoza katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni kwa kiwango cha asilimia 25, na kwamba mchango wa tasnia ya utalii kwenye pato la Taifa sasa umekadiriwa kupita asilimia 17. Aidha, takwimu zinaonyesha kuwa utalii umeajiri wafanyakazi 500,000 (direct employment), na zaidi ya watu 2,000,000 wananufaika na biashara ya Utalii kwa namna moja au nyingine. Wawakilishi wa Balozi mbalimbali zilizopo nchini wamewahi kusema “ watawaalika wawekezaji kutoka nchi zao watumie fursa zilizopo katika Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) ili kukuza sekta ya Utalii. Tanzania inatakiwa kuiweka sekta ya Utalii kuwa miongoni mwa vipaumbele vyake katika kuingiza fedha za kigeni.

Mbe. Lazaro Samuel Nyalandu (MB)



Rais wa Awamu ya Pili, Mhe Ali Hassan Mwinyi

“There is not an animal that lives on the earth, nor a being that flies on its wings, but they form communities like you. Nothing have we omitted from the Book, and they all shall be gathered to their Lord in the end” (Quran 6:38)

Jinsi wanyama wetu katika mbuga za wanyama wanavyogombaniwa ni jambo la kuangaliwa kwa umakini na kuchukua hatua za haraka. Nilipokipitia kwa kukisoma kitabu hiki, nimekumbuka kitu kimoja, wageni tunaowapatia nafasi katika mbuga zetu kufanya utalii na pia wakati mwingine kufanya uwindaji, wanavyowagombania wanyama walioko katika mbuga zetu maana huko kwao wamewamaliza wote!

Sasa hivi kuna tishio kubwa la ujangili, kwa tembo na faru, kinachotafutwa kwa wanyama hawa si kitoweo, bali pembe zao, bila kukomesha tabia hii ovu ya uuaji wa tembo na faru

Tanzania iko hatarini kuupoteza urithi huu ambao Mungu ametupatia vizazi na vizazi. Watalii wanaposafiri hasa kutoka Nairobi na kupita Maasai Mara National Reserve magari ya wazi wanaona utajiri huu aliotuachia Mwenyezi Mungu, na wanabaki wakishangaa.

Sikustaajabu kuona viongozi wa Dini wa Kamati ya Amani ya Mkoa wa Dar-es-Salaam nao walipotembelea baadhi ya mbuga zetu kupatwa na mshtuko, wakijiuliza kama kasi ya kuua tembo na faru itaendelea hivi, matokeo yake yatakuwa nini? Na pia natumaini walijiuliza maswali mengi na moja ya maswali natumaini moja wapo ni hili! Je wanaoshirikiana kufanya tendo hili si ni Waislamu na Wakristo? Mbona watu hawa wanaenda Makanisani na Misikitini kuabudu!

Yawezekana kabisa jamii inahitaji kukumbushwa, na wakufanya hivyo ni viongozi wa dini zote! Ulimwengu sasa umekuwa kijiji, lakini hatuna budi kukataa kumezwa na utandawazi! Yapo makabila ambayo yameishi na wanyama karne na karne wamekuwa na utaratibu wa kuishi, hawakuu wanyama ovyo, bali wamekuwa na utaratibu wa kiuumbaji, Wamasai wanaweza hata kugawana nyama na simba aliyeua nyati bila madhara yoyote.

Tujifunze sasa, kwamba idadi ya watu inaongezeka, njia mojawapo itakayotusadia sisi na wanyama pori kila mmoja kuishi katika himaya yake ni kujenga makazi ya kisasa kwa mpango endelevu, makazi yanayoweza kuchukua watu wengi na kuwapatia huduma za kijamii bila shaka yoyote.

Kuwa na vijumba vidogo vidogo, na kuzisogelea mbuga za wanyama ni jambo ambalo tunaweza kabisa kupata ufumbuzi wake. Jamii inayokaa karibu na mbuga hizi lazima inufaike na mazao ya mbuga za wanyama.

Ali Hassan Mwinyi - Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania -Dar-es-Salaam. 2015

QUOTABLE QUOTES



Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere

“The survival of our wildlife is a matter of grave concern to all of us in Africa. These wild creatures amid the wild places they inhabit are not only important as a source of wonder and inspiration, but are an integral part of our natural resources and our future livelihood and well being. In accepting the trusteeship of our wildlife we solemnly declare that we will do everything in our power to make sure that our children grand-children will be able to enjoy this rich and precious inheritance” Arusha Manifesto; 1961.

“Nyerere philosophy to protect and cherish Tanzania’s spectacular wildlife as a prime national heritage is expressed in the high priority the Tanzanian government has given to conservation of natural resources”

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

UTANGULIZI

Kitabu hiki ni matokeo ya ziara ya Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini Mkoa wa Dar-es-Salaam. Inawezekana hata viongozi wenyewe wa dini pamoja na mwandishi hakuna aliyekuwa na lengo la kuwepo kwa uandishi wa kitabu hiki cha kihistoria, hapo ndipo unapoweza kushangaa mipango ya Mungu.

Wakati viongozi hawa wa dini wanatembelea mbuga za wanyama, Tarangire na Arusha National Park, walijionea kwa macho yao utajiri ambao Tanzania inao, kwamba kama ukitumika vizuri, nchi hii, hasa katika Afrika Mashariki, hakuna nchi ambayo inaweza kuifikia katika miaka inayofuata.

Ujangili una athari kubwa kwa taifa letu, Serikali imekiri wazi kuwa ongezeko la ujangili ni chanzo kikubwa kinachodhoofisha sekta hii ya utalii nchini na kudidimiza uchumi wa taifa. Hii ni vita! Hasa ukiangalia kuwa katika Afrika Mashariki ni Tanzania peke yake yenye eneo kubwa la mbuga za wanyama.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dr Adelhelm Meru amekiri wazi kuwa, upo uwezekano ujangili ukaathiri ajira zipatazo milioni 3.8. Hii ina maana gani? Viongozi wa dini tuliona vijana walio na mafunzo mazuri ya kuongoza watalii, madereva, hoteli za kisasa zilizopo katika mbuga hizi, wahudumu waliopo katika migahawa wanavyoyakabili maisha yao kwa ajira hii, sasa unaweza kujiuliza, kama wanyama watatoweka hawa wote wataenda wapi?

Katika miaka 10 iliyopita, Tanzania pamoja na nchi nyingine za Afrika zimeathirika kwa kiwango cha kutisha kutokana na ujangili. Kitakwimu na kiutafti ambao umefanyika mwaka 2014, Tanzania imepoteza zaidi ya nusu ya tembo kutoka 110,000 mwaka 2009 hadi 44,000.

Faru wamepungua, twiga ambao ni alama ya Taifa nao wamepungua kwa kiasi cha kutisha. Majangili wao hawajali kabisa athari ambazo taifa linakabiliana nazo! Hapa ndipo unapona umuhimu wa viongozi wa kiroho kuingilia kati!

Mungu ameweka utaratibu wa mzunguko wa maisha. Ndio maana ukienda katika mbuga za wanyama huwezi kukuta simba akiua wanyama wengine hovyoyoy, au ameu mtoto wa swala, umewahi kujiuliza toka umezaliwa lini ulikosa nyama ya ng'ombe, mbuzi, kondoo! Kwa wale wanaoishi kando kando ya bahari, mito na maziwa lini wamekosa samaki?

Mashirika ya Wildaid na African Wildlife Foundation wamekuwa wakifanya kazi bega kwa bega na serikali yetu, katika kampeni ya “ Ujangili Unaatumiza Sote” kwa

ushirikiano na Wizara, na Viongozi wa Dini, pamoja na wana siasa, watu wa sanaa, mashule, vyyuo vikuu, jamii itapata uelewa kuhusu ujangili kwamba ni janga la Taifa.

Viongozi wa dini, kwa kutumia maandiko Matakatifu, wataweka katika mioyo ya watu hofu ya Mungu, na kwa sala na maombi ya kila siku watu watabadilika. Watanzania hatuna budi kuelewa kuwa, ujangili ni uuaji! Ni wizi, hauna tofauti na mtu anayevunja duka na kuiba mali ya mwenye duka! Watanzania wote, kwa umoja wetu, hatuna budi kuungana katika vita hii.

Utalii uivutie jamii, watu waone kwamba vivutio vya utalii ni mali ya Watanzania. Watu waelimishwe kutunza na kuanzisha vituo vya utalii. Hii ni sehemu ya ajira. Kumheshimu Mungu ni kumtii, kuacha kabisa ukatili wa aina yoyote ile kwa wanyama wa kufugwa na wale wa porini.

Wakati utakapokuwa unasoma kitabu hiki, fikra zako zibadilike kuwa wewe ndiye mtu muhimu kukemea ujangili, tunatakiwa kuheshimu kile ambacho Mungu ametupa, tukitunze, tuwe mawakili wema, kuutunza uumbaji, ili nao ututunze.



Mchungaji Christosiler Petro Kalata

Mwandishi wa Kamati na Mjumbe Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Dar-es-Salaam

Tanzania's religious leaders join the fight to save the elephants - February 17th 2015



Mr. Peter Knights, CEO of WILDAID

Tanzania is the epicentre of Africa's elephant poaching crisis. Two-thirds of the country's elephant population has been wiped out since 2006, according to a recent report. Rhino populations are even more imperilled, their total numbers in Tanzania having fallen to around 30, according to recent news reports.

Tanzania is a deeply religious country, and faith leaders have a great influence on the lives of its citizens across the social strata. That's why WildAid recently organized an interfaith workshop, to work closely with prominent religious leaders who share a deep concerns about the future of Tanzania's wildlife.

As one attendee put it, "When you involve religious leaders, you avoid using guns and prisons as a means of enforcement. The people living in those communities are our people and our responsibility. We have the ability to reach them much faster than any radio or television station."

"As religious leaders, you have the power and the opportunity that the government doesn't," Minister Nyalandu told the attendees. WildAid presented on the scope and severity of Tanzania's poaching crisis for both elephants and rhinos, and showed examples of its PSAs that discourage the buying of ivory and rhino horn.

The faith leaders were outraged by the scale of the problem, and they took the opportunity to stress to Minister Nyalandu the need for better communication, stronger enforcement measures and harsher criminal penalties for poaching.

Elephants and other animals are citizens of this country. They have a right to live here," said Bishop Valentino Mokiwa of the Anglican diocese of Dar es Salaam. "These animals are made by God for the good of human creation. Even though elephants cannot vote, they can have an influence over who becomes our next President."

Sheikh Alhad Musa Salum stated that "As human beings, we must be good to these animals, despite hard financial difficulties and the high rate of unemployment in this country," he said.

SHUKRANI

Mafanikio ya Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Da-es-Salaam, ni matokeo ya ushiriki wa Viongozi wa Dini wa Madhehebu mbalimbali, ushiriki wa watu wengi tunaowafahamu na tusiowafahamu. Kitabu hiki ni matokeo ya mengi tuliyojifunza kutoka katika ziara mbalimbali, washa, na semina. Kutembelea mbuga za wanyama, Tarangire na Arusha National Park, kuliamba ari ya kuwaeleza wanadamu kuwa uumbaji wa Mungu una makusudi na ni mpango maalum kwa maisha ya viumbe na wote wanaoishi katika dunia.

Watanzania wote wa dini zote, serikali, asasi mbalimbali, wanasiasa, wanaharakati, Maprofesa wa Vyuo Vikuu, Mawaziri, Wabunge na kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Profesa. Jakaya Mrisho Kikwete, viongozi wa dini wanasema Amani na Usalama si kwa wanadamu tu bali hata kwa viumbe alivyoviumba Mwenyezi Mungu, hata sisimizi anahitaji kuishi, maana hakuna mwanadamu anayeweza kumwumba.

Ni vigumu mno kutaja jina la kila mmoja aliyeshiriki katika kufanikisha kazi hii njema, tunawiwa kuwataja wachache wafuatao:- Sheikh Abubakar Zuber - Mufti, Sheikh Ally Basaleh - Hyyat Eulamaa, Sheikh Ally Muhidin Mkyogore - Naibu Kadhi, Askofu Dr Valentino Mokiwa - Mkuu wa Dayosisi ya DSM - Anglikani, Askofu Dr Alex G. Malasusa - KKKT - Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Mch George Fupe, Askofu Steven Mangana - Askofu Mkuu Kanisa la Menonight, Sheikh Abdulrahama Ally Issa- Imam, Canon Thomasi Godda - Mkurugenzi - IRCPT, Askofu Philemon Phili-EAGT, Askofu Tibananason - Mwenyekiti wa Maaskofu wa Pentekoste-DSM, Mch Amani Lyimo - M/Kiti - Umoja wa Makanisa - DSM, Sheikh Juma Bin Sadiq -Taasisi Muhibu Rasul, Sheikh Othman Mataka - M/Kiti ALMALD, Sharifu Abdulkadir Hussein (caba Scuba) Rais Jumuiya ya Waislamu-Kigamboni, Askofu Silvester Gamanywa - WAPO Mission, Mtume Josephat Mwingira - Kiongozi wa Ephata - Ministry,

Mtume Venon Fernandes - Agape Ministry, Sheikh Ismail Makusanya - Sheikh Mkoa wa Shinyanga, Sheikh Saleh Omary - Naibu Katibu Istiqama Taifa, Sheikh Khamisi Abasi Mtupa - Kadhi Mkoa wa Pwani, Sheikh Athmani Mkambaku - Naibu Katibu Kamati ya Amani, Sheikh Khamis Hussein Mtonga - M/Kiti wa Vijana wa Kiislamu Mkoa wa DSM.

Sheikh Alhad M. Salum

Mwenyekiti, Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini wa Mkoa wa Dar es Salaam

SURA YA KWANZA

SIKU YA SITA YA UUMBAJI

“Mungu akafanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake, na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake, na kila kitu kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema” Mwanzo 1 : 25

Ni jambo muhimu kwa mwanadamu kutafakari kazi ya Mungu kuhusu uumbaji. Mwanadamu anatakiwa kujifunza juu ya maajabu ya Mungu. Kazi za Mungu za ajabu zinazoonekana katika uumbaji na katika historia, ni sababu ya kuuheshimu uumbaji, kuisifu kazi ya Mungu, kumwabudu na kumtukuza kwa kazi yake njema.

Watu wakiitikia wito wa Mungu, Muumba atawabarikia, atawapa uzao bora! Watu watakuwa wenye mafanikio. Kutoka mashariki hadi magharibi, wakati huu tulionao na wakati ujao, Mungu anastahili kuabudiwa na watu wote.

Biblia sio kitabu cha kufundisha sayansi, Biblia inayatazama mambo kwa njia ya kipekee sana, kuhusu mwanadamu na wanyama pamoja na viumbe wengine wanaojaza dunia hii, mwanadamu ni kiumbe cha pekee sana, Biblia inasema juu ya mbingu na nchi kama zinavyoonekana kwa watu wanaokaa katika dunia hii.

Kabla ya miaka isiyohesabika, Mungu aliziumba mbingu na nchi, yaani ulimwengu wote kwa kutumia uwezo na mamlaka yake. Uumbaji wa Mungu ulipoendelea wanyama wa kila aina walitokea, wakakuta mazingira yaliyowafaa, hasa viumbe vya baharini na nchi kavu.

Uumbaji wa mwanadamu umekuwa wa kipekee, maana alipewa uwezo wa kumiliki. Ni katika upekee huu mwanadamu aliandaliwa makazi bora ya kukaa, na kuufurahia uumbaji, na sio kuufurahia tu bali kuwa mtu wa ibada na kuwa wakili mwema.

Siku ya sita ya uumbaji, tunaona kuwa Mungu alipumzika. Hii haina maana kuwa Mungu alikuwa amechoka!

Mwanadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu, bila hivyo mwanadamu asingekuwa mwanadamu! Angefanana na mnyama. Unyama wa mnyama uko katika hali na tabia yake mwenyewe, mwanadamu ana utu, asili ya kimungu iko ndani yake. Mungu amempa heshima ya hali ya juu mwanadamu.

“Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi ”. Mwanzo 1 : 27-28.

Msingi wa mambo yote yanayomuhusu mwanadamu ni ule upekee wake wa kiuumbaji kwamba Mungu amemuumba kwa ustadi mkubwa. Kwa hiyo mwanadamu ni kiumbe cha pekee kati ya viumbe vyote. Mungu toka uumbaji amempa mwanadamu mamlaka ya kutawala, kumiliki, kutumia kwa utaratibu vitu alivyopewa kumiliki kwa utaratibu wa kiuumbaji. Upekee wa uumbaji haujaribiwi kumgawa mwanadamu katika sehemu mbalimbali za kimwili, ziwe ni za kiroho, za maadili, za mawazo, za hisia na kadharika, sababu ni moja tu! Mwanadamu ni umoja kwa ujumla wake. Quran inasema:

*“There is not an animal that lives on the earth, nor a being that flies on its wings, but they form communities like you. Nothing have we omitted from the Book, and they all shall be gathered to their Lord in the end”
Quran 6 : 38*

“Once someone travelling with the Prophet took some eggs from a nest, causing the mother bird great grief. The Prophet saw this and told the man to return the eggs.”

“When the Prophet was asked if Allah rewarded acts of charity to animals, he replied: “Yes, there is a reward for acts of charity to every beast alive.”

“It is God who provided for you all manner of livestock, that you may ride on some of them and from some you may derive your food. And other uses in them for you to satisfy your heart’s desires. It is on them, as on ships, that you make your journeys. Qur’an 40:79-80

“What is the matter with you that you hope not for greatness and wisdom from Allah? And He has created you in different forms and different conditions. See you not how Allah has created seven heavens in perfect harmony, and has placed the moon, therein a light and made the sun a lamp? And Allah has caused you to grow out of the earth as a good growth. Then will He cause you to return, thereto, and He will bring you forth a new bringing forth “ (71:14-19)

O you human beings! What is the matter with you that you fail to understand that Allah does not do anything unless there is wisdom and purpose underlying it? You yourselves are not ready to accept the assumption that you do things with no aim or purpose in view.

Why do you therefore assume that Allah, the Most Wise and All Knowing does things without purpose? Why do you jump to the thoughtless conclusion that He created man with no purpose in view? Why do you fail to grasp the evident truth that your creation has not been the result of a sudden meaningless impulse?

It was the result of wise planning and deliberate execution in a succession of stages from one point to another. Do you not see that Allah has created the seven heavens in perfect harmony with each other and similarly the sun and the moon?

Also that the earth was one of the stages through which you passed in a process of slow growth to the point of perfection?

Mwanadamu anazo sababu nyingi za kuwa na furaha ambazo hana budi kuziweka katika akili yake, ambazo hakuna mtu awezaye kuziondoa.

Mungu ameumba ulimwengu wenye vitu vingi vizuri ametupa ili tuvifurahie. Hakutuacha hivi hivi ametupa kazi ya kufanya na anategemea uaminifu wetu! Amani ni kitu kinachotakiwa sana katika maisha ya mwanadamu na wanyama.

“Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani ; vile vile kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu ” I Kor 14:13

Wakati mapenzi ya Mungu yanapofanyika kunakuwa na amani katika vitu vyote. Wanyama hufurahia umoja wao, kila mmoja akimjali mwenzake.



Lakini dhambi imeingia duniani na mapenzi ya Mungu hayatimizwi. Na mahali ambapo mapenzi ya Mungu hayatimizwi kuna ugomvi. Mtu alizaliwa kuwa rafiki wa Mungu, lakini amekuwa adui wa Mungu na wanyama pia.

Muslim Statement on conservation of wildlife:

“The animals and insects play a vital role in the ecosystem of the earth. These species should be respected, protected and not to be destroyed. If a species become extinct it can never, ever be replaced and a whole ecosystem with many lives can be affected”



Uuaji wa aina yoyote ile haukubariki! Ninaposema uuaji maana yake ni kuutoa uhai wa kiumbe kinachoishi pasipo mapenzi ya Mungu. Mungu amempa mwanadamu kutawala, kutumia, na kutunza, wala si kuharibu!

Kila kiumbe kimewekwa mahali pake kwa mpango maalum, hata siafu ana umuhimu wake! Kuchoma msitu moto ni uuaji, maana kuna viumbe vinateketea, ambavyo hakuna mwanadamu anayeweza kurejesha uhai wake.

Ni muhimu kwa mwanadamu akumbushwe wajibu wake katika maisha yake hapa duniani! Kwamba kila anachokiona katika ulimwengu huu ni mpango kamili wa Mola! Ni dhambi kubwa mno kuondoa uhai wa kiumbe chochote kile!

Kama mwanadamu atakuwa na utulivu, na kuutafakari uumbaji wa Mungu ataacha kiburi! Maana ikiwa wadudu wadogo wanaweza kushirikiana kufanya kazi, kulikoni wewe mwanadamu uliyeumbwa kwa upendeleo wa hali ya juu, kupita hata malaika.



It is important that humankind does not become a perpetrator of this great sin. The animals and the insects have a right to share mother earth with humankind.

Uumbaji huu ni upendo mkubwa wa Mungu kwa mwanadamu, Mungu hakutaka mwanadamu awe mpweke aliweka viumbe mbalimbali vilivyomzunguka.

Wanyama wa kila aina hata wale ambao unaweza kufikiria kuwa hawana faida yoyote kwako, Mungu anawajali mno! Baada ya uumbaji Mungu aliona kila kitu ni chema na kina faida, basi usimwone Mungu kuwa ni mpumbavu kuweka vitu vya aina hiyo!

Usiyaharibu mazingira yasije yakakuharibu, ukitaka maisha bora yatunze mazingira! Utafurahia uhai aliokupa Mwenyezi Mungu!



“God said, See, I have given you every plant yielding seed that is upon the face of all the earth, and every tree with seed in its fruit; you shall have them for food. Genesis 1:29



Usistaajabu kuona mimea ya asili ikiota kila mahali pasipo juhudi yoyote ya mwanadamu! Huo ndio uumbaji wa Mola! Hakika mwanadamu kama angetaka kuifanya kazi hii, ingemgharimu kiasi kikubwa cha fedha na bila kupata mafanikio yeyote!

Mwanadamu atahukumiwa kwa mambo ambayo kwa matendo yake aliyotenda, moja likiwa uharibifu wa mazingira.



“Wana simba hunguruma wakitaka mawindo, ilikutafuta chakula chao kwa Mungu. Jua lachomoza, wanakwenda zao, Na kujilaza mapangoni mwao” Mwanzo 104:21-22

Kwa sababu ya utawala wa Mungu, dunia inatoa chakula kwa wanadamu na wanyama, nao wanapewa mahitaji yao yote ili waweze kuishi kwa usalama.

Yeye anapanga misimu na hali ya hewa, usiku na mchana, hata mahitaji ya aina yote ya maisha yaweze kutimizwa. Hakuna haja ya kumtilia mashaka Mungu! Mashaka ya mwanadamu yako katika moyo wake mwenyewe.

Mungu anayajua mahitaji yetu! Ndiyo maana ametupatia kila kitu sawa sawa na uhitaji wetu, kinachoshangaza ni pale tunapomlazimisha atupe kile tunachokitaka hata kama kitatuletea madhara makubwa.

Lakini Mungu ni mwema wakati wote, anatu pusha na hatari nyingi, maana anatumia ubinadamu wetu! Laiti tungalijua ustadi wa Mungu aliotupangia katika maisha yetu hapa duniani tungejipusha na majanga ya kujitakia yanayotokea leo.

BAADA YA UUMBAJI

Maandiko Matakatifu kutoka vitabu vyote, Biblia na Quran yanaonyesha kuwa baada ya uumbaji Mola alimpa mwanadamu dhamana kubwa! Kutunza.

Mwanadamu anatakiwa kuwa wakili mwema, kwa kila kitu kilichoumbwa na Mungu na kuwekwa katika milki yake!

Quran speaks of Humankind as vice-regent. He does not own the earth, to do with as he pleases, but must care for the creation in Allahs name. Hapa utaona jinsi mwanadamu alivyopewa heshima kubwa kuzidi viumbe vyote duniani, inashangaza mtu kuupoteza utu wake kufikia hatua anafanya kama mnyama anavyofanya!



Baada ya Mungu kuifanya kazi yake ya uumbaji kwa ustadi mkubwa. Kuumba vitu vyote, vile vinavyoonekana na visivyoonekana hata na vile viumbe vya kiroho, ingawa labda vilikuwepo hata kabla ya ulimwengu unaoonekana, ni viumbe vilivyoubwa na Mungu.

Ni vigumu sana kuelewa viumbe katika ulimwengu wa roho!

Maandiko yanasema *“Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema, kama ukiwa na ufahamu. Ni nani aliyeamrisha vipimo vyake, kama ukijua? Au ni nani aliyenyosha kamba juu yake? Misingi yake ilikazwa juu ya kitu gani? Ayubu 38:4-6*

Mara kadhaa Ayubu alikuwa amemwita Mungu ashindane naye kwa majadiliano. Mara zote Mungu hutualika tujadiliane naye.

“Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe; wala sitazikumbuka dhambi zako. Unikumbushe; na tuhojiane; eleza mambo yako, upate kupewa haki yako” Isaya 43:25-26.

Mungu bado anataka kuwasamehe watu wake wakijichunguza tu na kukubali makosa yao. Ujangili unaofanywa kwa tembo na faru katika nchi ya Tanzania na Afrika kwa kwa ujumla, ni dhambi na ni uasi kwa Mungu, tunahitaji kutubu! Mungu anaingalia Tanzania na Afrika kwa upendo mkubwa, anahitaji watu watakao tubu kwa dhambi hii ya ujangili.

“Na kheri yoyote watakayoifanya hawatakanushiwa (thawabu zake). Na mwenyezi Mungu anawajua wanaomcha (wakajiepusha na makatazo Yake na wakafanya maamrisha Yake na wakafanya maarisha Yake). 3:115

Hapa inabainishiwa kuwa yoyote Yule anayefanya mema kwa (a) Nia nzuri na (b) Kufuata alivyosema Mungu atalipwa tu mema. Ama asiyemkubali Mwenyezi Mungu wala amri Zake na makatazo Yake, hata akifanya mema hana jaza huko Akhera.

Akistahiki kulipwa atalipwa papa hapa tu basi.

“Na kila kilichomo mbinguni na kilichomo ardhini ni cha Mwenyezi Mungu; na mambo (yote) yatarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu.”

Mwanadamu anaamrisha kutenda yaliyo mema. Na anakatazwa kutenda yaliyo maovu. Mungu anamkusudia mwanadamu aishi katika uhusiano mzuri na Muumba wake, na wanadamu wenzake, na mazingira yake na nafsi yake mwenyewe.

Mwanadamu anatakiwa awatunze wanyama wa porini, hifadhi ya wanyama, mbuga za wanyama, ni mandhari ambayo Mungu ameiveka katika nchi kwa kusudi la kuweka mzunguko wa maisha endelevu.

Viongozi wa kiroho kwa jambo hili la ujangili hawapaswi kukaa kimya hata kidogo. Dhambi hii inalitafuna taifa, ni ugonjwa wa kuambukiza lazima utafutiwe tiba. Kwa kweli Watanzania hatuna tabia ya ujangili, ujangili umeingia Tanzania na Afrika kwa staili ya ajabu sana, kupitia umaskini, watu wametumika kuharibu vitu vya thamani alivyotupa Mungu.

Mungu baada ya kuumba vitu vya asili, aliendelea kuvitumia vitu vile vya ulimwengu wote pamoja na vile vya angani kwa kuendeleza na kufanya vitu vingine kwa sura zake. Aliumba wanyama na wanadamu kutokana na vitu alivyokuwa ameviumba kabla.

Biblia inasema *“Bwana wetu ni mkuu na mwingi wa nguvu, Akili zake hazina mpaka. Bwana huwategemeza wenye upole, Huwaangusha chini wenye jeuri... Humpa mnyama chakula chake, Wana-kunguru waliao” Zaburi 147:5-9*

Mungu anafurahi kutoa mahitaji kwa viumbe vyote. Viumbe vyote vinaonyesha maajabu ya Mungu, na kwa kufanya hivyo vinamsifu. Kuanzia vile vilivyopo juu kabisa, kama vile malaika, mpaka wanyama wote wa duniani, sifa zinapanda hata zimfikie huko juu. Kuanzia juu kabisa angani hadi vilindini vya bahari.

“Niende wapi nijiepushe na Roho yako? Niende wapi niukimbie uso wako? Kama ningepanda mbinguni, wewe uko; ningefanya kuzimu kitanda change, wewe uko” Zaburi 139:7-8

The nature of the Universal Mind is Omniscience (all knowing), Omnipotence (all powerful), Omnificence (all creative) and Omnipresence (always present).

Know that this too is your nature. You have access to all knowledge, known and unknown; you have access to an infinite power for which nothing is impossible; you have access to the limitless creativity of the One Creator.

All these attributes are present within you at all times in their potential form. Mungu alikuwa na makusudi yake, na alikuwa na mpango kamili, alipomwumba mwanadamu, vivyo hivyo alipoona kuwa ni vyema wanyama wawepo! Mpango wa Mungu ni mwanadamu atawale mbingu na nchi pamoja naye.

Mungu aliumba vitu vingi, vya ajabu sana! Kati ya viumbe hivyo ni malaika, malaika walikuwa na kazi moja kubwa kufanya mapenzi ya Mungu. Malaika humwabudu Mungu na kumtumikia kwa kuhudumu.

They do not eat or drink. The angels do not get bored or tired of worshipping God:

“They celebrate His praises night and day, nor do they ever slacken.” (Quran 21:20)

The angels possess great powers given to them by God. They can take on different forms. The Muslim scripture describes how at the moment of Jesus' conception, God sent Gabriel to Mary in the form of a man:

"...Then We sent to her Our angel, and he appeared before her as a man in all respects." (Quran 19:17)

Mungu alimuumba mwanadamu kwa mpango maalum, ndio maana utaona kila taifa, katika mazingira tofauti tofauti, watu wanapata mahitaji yao.

Wazo lolote la uharibifu, halitoki kwa Mola. Uharibifu umu ndani ya moyo wa mwanadamu mwenyewe! Kumuondoa mwanadamu katika uovu lazima umjengee asili yake ya Kimungu.

Wazo la Uumbaji

The idea of Creation is one of the main distinctive marks of the Christian mind. It was foreign and alien to the Greek mind. Perhaps, the true point of discrimination between the two systems was exactly this idea of Creation.

"Bwana Mungu akasema, si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. Bwana Mungu akamfanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake" Mwanzo 2:18-19

Mwanadamu aliumbwa na Mungu, kwa hiyo hakuna kiumbe kingine duniani kilichoweza kushiriki naye kimaisha kwa njia ya kumridhisha. Hivyo Mungu alimpa mwenziwe wa aina yake, lakini kwa hali ya kimwili, mwanamke.

Ili awe mwenzi wake. Mwanamume na mwanamke waliunganishwa kwa hali ya amani na kupatana, kwa jinsi isivyowezekana kwa viumbe vingine vyote.

Mwanamke baadaye alipewa jina la Hawa, maana yake "maisha" au "kuishi" kwa sababu kwa njia yake baadaye uhai wa binadamu ungetokea. Maajabu makubwa ya Mungu!

Prophet Muhammad (SAW) said: *Treat women kindly. Woman has been created from a rib and the most crooked part of the rib is the uppermost. If you try to straighten it, you will break it and if you leave it, alone, it will remain crooked. So treat women kindly. (Bukhari and Muslim)*

Kwa namna yeyote ile mwanamke asifanywishe kazi za kiume, mwanamke ni chombo cha aina yake, ndiyo uumbaji wake Mola, ana aina ya sauti ambayo haipatikani kokote, wala hakuna kiumbe chochote kinachoweza kufanana naye.

Kusudi la Uumbaji


Mungu alipowaumba Adamu na Hawa watu wa kwanza kabisa, mume na mke, aliwapa mamlaka juu ya nchi na aliwaambia waitunze na kuiweka chini ya utawala wake

“Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana, Dunia na wote wakaa ndani yake. Maana ameiveka misingi yake juu ya bahari na juu ya mito ya maji aliithibitisha” Zaburi 24:1-2.

Mungu, amempenda mno mwanadamu akampa kila kitu; kwa tabia aliyonayo mwanadamu, hawezi kumkaribia Mungu, maana uovu upo katika asili yake. Ndio maana mwanadamu huwa anajiuliza “ Nani anaweza kumkaribia Muumbaji Mwenye Mamlaka yote “ Jibu mara nyingi linakuwa hili “ Mtu Yule tu ambaye ana mikono safi “ katika shughuli zake zote na wanadamu wenzake na mwenye moyo wa kuwapenda wenzake na vitu vinavyomzunguka, wakiwemo wanyama “ Usalama wa Mwanadamu, na wanyama uko mikononi mwa Mungu!

Shetani na roho wake wachafu ni adui mkubwa wa binadamu wapo duniani! Mwanadamu hakuumbwa na roho chafu, roho ya mauaji, roho ya ujangili haikutoka kwa Mungu bali kwa Shetani! Unapomwona mwanadamu anafanya ubaya maana yake ametii maagizo ya Shetani! Kuamini uongo wa Shetani hupelekea kumwamini eti atakupa vitu vyote vya duniani!

Pengine tujiulize swali; Je Shetani ana kitu chochote alichokiumba? Hana hata kitu kimoja! Nguvu na utawala wa Shetani umo katika nafsi ya mwanadamu, ndiyo maana utaona ulimwengu kumejaa dhambi, ikiwemo ya ujangili, nina shaka, kama uongo huu wa Ibilisi ungepitiliza na kusema “ Meno” ya mwanadamu yana thamani inayopita ile ya pembe za tembo na faru!



After Adam had learned the names of all things, along with their properties and uses, Allah presented them to the angels and said: “Tell Me the names of these if you are truthful.” [Ch 2:31 Quran] the angels admitted their inability: “Glory be to You, we have knowledge except what You have taught us. Verily it is You the All Knower, the All Wise.” [Ch 2:32]

Kitu cha kwanza kabisa, makaburi yote yangefukuliwa, na pili mtu akifa wanadamu wangehakikisha wanayang’oa meno yote ya maiti na kumfunga mdomo wake kwa ustadi mkubwa! Mioyo ya wanadamu, mahali pote mioyo ya wanadamu, imejawa na: Kuabudu sanamu, Uchafu, Aina zote za Uovu.

“Kwa sababu, walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru; bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo. Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tama za mioyo yao, waufuate uchafu, hata wakavunjiana heshima miili yao kwa maana waliabadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina ” Rumi 1:21-24

Ni ajabu sana, badala ya kutunza watu wanaharibu, huku ni kumchukiza Mungu, Mungu anachukia dhambi ya ujangili, na aina zote za dhambi. Inawezekana kwamba mataifa hawakupata mafundisho juu ya utunzaji wa mazingira.

Utunzaji wa wanyama, samaki wa baharini na viumbe wengine wengi, ni wajibu wa mwanadamu. Hata sisimizi wanahitaji kuishi! Mwanadamu hana cha kujitetea kwamba hamjui Mungu! Mungu ndiye aliye waumba pamoja na viumbe wengine, hii inaonyesha kwamba yuko Muumbaji, Mwenye uwezo, ambaye inampasa mwanadamu amwabudu huyo peke yake.

Ni ajabu sana, badala ya kumpa Mungu utukufu, watu wanamchukiza, kwa kuua viumbe visivyo na hatia yoyote! Badala ya kumwabudu kama Muumbaji, walifanya viumbe kuwa miungu yao. Wanadamu wanajidai kuwa na akili nyingi kumpita Mungu. Lakini ukweli ni kwamba ni wa wajinga. Wanadamu wanatenda uovu mchana kweupe, bila kuogopa adhabu ya Mungu.

Mungu anaangalia tu dhambi zao, na njia moja ya kuwadhibu ni kuwaacha wajiangamize kwa kufuata tamaa zao mbaya za dhambi. Na watavuna matunda ya dhambi zao! Viongozi wa dini mbalimbali katika mahubiri yao wanatakiwa kumuonya mwanadamu kuuacha uovu, vitendo viovu vinavyomchukiza Mungu. Ni ajabu kumuona mwanadamu anafanya uovu uliopitiliza.

Mazingira ya Uumbaji

“Ee Mungu, unirehemu, sawasawa na fadhili zako, kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu. Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu” Zaburi 51:1-2

Baada ya kuona kwamba Mungu ametuwekea mazingira mazuri na sisi tumeyaharibu tunatakiwa kutubu. Hatuna chochote cha kujitetea, tumejawa na uharibifu uliopitiliza, wanadamu tumeendelea kuharibu uumbaji, tukubali makosa yetu, hatuna njia nyingine, tukubali kwamba ujangili ni kosa mbele za Mungu, sasa tujikabidhi kabisa katika huruma ya Mungu isiyo na kikomo.

“Maana nimejua mimi makosa yangu, Na dhambi yangu mbele yangu daima. Nimekutenda dhambi wewe peke yako, Na kufanya maovu mbele za macho yako. Wewe ujulikane kuwa Una haki Unenapo; Na kuwa safi utoapo hukumu” Zaburi 51:3-4

“In the name of God, the Merciful and Compassionate: praise belongs to God, the Lord of the Worlds, the Merciful, the Compassionate; Master of the Day of Judgment, You do we worship and You do we call on for help; guide us on the Straight Path, the path of those whom You have blessed,

not of those who earn your anger nor those who go astray” (Quran 1:1-7)

“Is not He, Who created the heavens and the earth Able to create the like of them? Yes, indeed! He is the All-Knowing Supreme Creator “ Quran

Mwanadamu anatakiwa kuukumbuka uaminifu wa Mungu, toka kuumbwa kwa dunia Mungu hajawahi kuvunja agano lake. Jiulize mwanadamu amemkosea Mola wake mara ngapi?

SURA YA PILI

KUUMBWA KWA MWANADAMU NI MPANGO WA MUNGU

Mwanadamu ni Mtawala

Maisha yako hayajaanza tangu ulipozaliwa, bali Mungu alikuchagua tangu asili kwa ajili ya jambo aliloliweka ndani yako tangu kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu.

“Neno la Bwana lilinijia, kusema, Kabla sijakuumba katika Tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa.” Yeria 1:4

Mungu alimwambia Yeria kwamba alimjua kabla hajamuumba tangu tumboni mwa mamayake, na kabla hajatoka tumboni alimtakasa. Mazingira aliyo nayo mtu yanaweza kumwongoza jinsi ya kuamua cha kufanya lakini hayo yote haijalishi ni mazingira yapi yanayokufanya ulivyo fahamu kwamba ulikuwepo hata kabla haujakuwepo hapa duniani na uliumbwa kabla haujaingia tumboni mwa mama yako. Mungu alikuwa na maandalizi mazuri kwa ajili yako.

Inawezekana Kuna mahali umezuiliwa huwezi kutoka na inatakiwa nguvu fulani ikukute pale ulipo ikupeleke uende mahali ulipokusudiwa kufika. Mungu aliliona hilo na akaamua kumuumba mtu kwaajili ya kuuruthi ufalme aliouweka tangu asili ili ufanyike kama nguvu kwa kuwawezesha watu wake kufikia makusudi aliyoyaweka ndani yao.

“Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.” Mwanzo 1:26

Mungu alisema na tumfanye mtu kwa mfano wetu na kwa sura yetu ili akatawale duniani awe mfalme. Unaweza ukajiuliza kama sote tukiwa watawala ni nani atakayetawaliwa, hilo haliwezi kuondoa lile kusudi la Mungu kwasababu yeye ndiye anayetupa namna ya kila mtu atawale eneo lake sababu ametuumba kwa mfano wake na yeye anatawala.

“Mbingu ni mbingu za Bwana, Bali nchi amewapa wanadamu.” Zaburi 115:16

Nchi hii tumepewa tuitawale na viumbe vyake vya baharini, angani na nchi kavu. Adamu alisahau kwamba yeye ni mfano na sura ya Mungu ambaye ni mtawala akautoa Ufalme wake kwa shetani. Adamu alipoutoa utawala wake kwa shetani alimfanya shetani aujenge utawala wake juu ya nchi na mwanadamu akawa mtumwa kwenye nchi yake, shetani alijenga dunia akiwa yeye kama mtawala.

*“And We have certainly honored the children of Adam and carried them on the land and sea and provided for them of the good things and preferred them over much of what We have created, with [definite] preference.”
Quran (17:70),*

Mungu alimfukuza Adamu nje ya bustani ya Edeni sababu alitenda kinyume na sheria yake, tunaona kwamba ukitenda kinyume cha sheria ya Mungu Mungu anakufukuza nje ya utukufu wake. The Quran states *‘Every soul shall bear its own burdens’ and ‘Nobody will carry anybody’s burden’ in the Quran (6:164).*

Kila mwanadamu atahukumiwa kwa kosa alilolifanya, sio kwa kosa la mtu mwingine! Jangili hakika atapata hukumu stahiki.

“Siku zile aliondokea Yohana Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema, Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.” (Mathayo3:2).

Mungu aliwarudisha wanadamu kwa kuwaambia watubu kwa maana Ufalme wa Mbinguni umekaribia/umefika. Yesu alifundisha kwa habari ya ufalme na akawafundisha wanafunzi wake jinsi ya kusali wakiwa ndani ya ufalme wa Mungu.

“Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.” (Mwanzo 2:7)

Roho ni mwanadamu halisi na huyu ndiye amekwisha kuandaliwa ili awe mtawala hapa duniani, huyu ndiye aliyetakaswa kabla ya kuzaliwa, kabla ya kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu.

Mwanadamu ana nafsi ambayo ni kiunganishi kati ya mwili na roho, nafsi ni daraja ambalo limeshika roho na mwili linaruhusu nguvu zilizoko kwenye roho ziingie mwilini kupitia nafsini, mtu anapokufa nafsi yake inapotea na vile vyote anavyovifahamu anaviacha hapa duniani. Nafsi ya mtu inaweza kufundishika ikambadilisha mtu na kuzimu inauwezo wa kuikamata nafsi ya mtu na kuiwekea elimu ya kuzimu ili mtu ajenge ufalme wa kuzimu hapa duniani.

Imeandikwa *“Uitoe nafsi yangu kifungoni. Nipate kulishukuru jina lako. Wenye haki watanizunguka, Kwa kuwa Wewe unanikirimu.” Zaburi 142: 7*

Mtu akiwa kifungoni anapewa mavazi ya kuvaa, anapangiwa muda wa kulala, anapangiwa chakula cha kula na kuna kazi za kufanya anapangiwa azifanye, anakuwa chini ya Bwana jela ambaye ndiye mwenye mamlaka juu yake na anapangiwa chakula cha kula hata kama hakipendi.

